

## Uvunaji

Uvunaji hufanywa baada ya ua kubadilika na kuwa manjano yaliyokoleza.

- Kata mazao yaliyokomaa na uyaanike juu-chini hadi yakauke kabisa.
- Saga maua hayo ya manjano kisha ukaushe mbegu kwenye jua.

## Ukaushaji

Tandaza mbegu kwenye chandarua kwa muda wa siku tatu au hadi mbegu ziwe laini.

## Kuhifadhi

Weka mbegu zilizokaushwa katika ghala lenye hewa kiasi. Wauzie mbegu wafanyi biashara ili kupunguza uharibifu baada ya mavuno.

## Mapato/Mavuno

Kwa kutumia mitindo inayo pendekezwa, mkulima anaweza kupata kati ya magunia 8 hadi 10 (ya kilo 50 kila moja) ya alizeti kwa kila ekari na kati ya magunio 25-25 (ya kilo 90) ya mahindi kwa kila ekari.

Mapato hayo yanaweza kumletea mkulima karibu shilingi 49,230 za Kenya (kulingana na bei ya mwaka 2008).



### Kenya Agricultural Research Institute

S.L.P. 57811, NAIROBI.

Simu: 254-20-4183301-20, Fax: 254-20-4183344

Baruapepe: resource.centre@kari.org

Tovuti: www.kari.org

### Watayarishaji:

Ojowi, M. na Okoko, N.

### Kwa maelezo zaidi, wasiliana na:

#### Mkurugenzi wa Kituo,

KARI-Kisii

S.L.P. 523 KISII

Kisii\_kari@yahoo.com

Vijitabu vya KARI vya taarifa, nambari / 66 /2008

**Shilingi 20 za Kenya**

## Ongeza mavuno ya Alizeti kwa kupanda mimea mseto



## Utangulizi

Alizeti ni mmea unaotumika sana kama mmea wa mafuta katika Kusini Magharibi mwa Kenya. Ni mmea wa mauzo ya thamani ya juu na hutoa mafuta ya hali ya juu.

Hata hivyo, ukuzaji wake ni wa kiwango cha chini kwa sababu ya kutumia mbegu duni, utunzaji mbaya wa mimea na kuliwa na ndege.

Wakulima wengi humiliki mashamba madogo madogo (ekari 1 hadi 3) na huwa na mtindo wa kupanda mmea kwa pamoja na mahindi kwa matumizi ya nyumbani na alizeti kwa mauzo.

## Faida za mseto wa mahindi – Alizeti

- Hupunguza hasara kutoka kwa ndege.
- Hupunguza utegemezi wa mahindi pekee.
- Kuimarisha ubora wa udongo na hivyo kuongeza pato kwa mazao mengi.
- Hupatia chakula kwa mifugo (ng'ombe na kuku).
- Husaidia uwekaji wa nyuki.
- Hupelekea matumizi mema ya sehemu ndogo za shamba.

## Matayarisho ya shamba

Tayarisha shamba mapema katikati ya mwezi wa pili (Februari) ili kupanda kati ya Machi na Aprili wakati wa mvua kubwa na katika Julai ili kupanda kati ya Agosti na Septemba.

## Kutenganisha

Mstari mmoja mmoja au miwili miwili ya mseto wa alizeti na mahindi inapandwa kwa sentimita 75x30.



Mseto mistari miwili ya alizeti

## Matumizi ya mbolea

Tumia mbolea ya nyumbani (viganja viwili kwa kila shimo), ongeza mbolea aina ya DAP vifuniko vya chupa viwili wakati wa kupanda.

## Upandaji

- Panda mbegu tatu za alizeti kwa kila shimo na mbegu moja ya mahindi kwa kila shimo.
- Ng'oa alizeti hadi usalie na moja kwa kila shimo baada ya matawi halisi.
- Panda mistari minne ya wimbi kandoni mwa shamba kama mistari ya kuzuia ili kuwakanganya ndege.

## Kupalilia

Limia majuma 2 hadi 3 baada ya kuota na urudie baada ya wiki 4 ama 5. Hii hufanywa ili kuipa mimea nguvu na mazao kuongezeka.

## Kupunguza mimea

Ng'oa mimea dhaifu ya alizeti baada ya kulimia ikiwa na urefu wa sentimita 15.

## Mbolea ya juu

Tumia vifuniko vya chupa viwili vya CAN karibu na mihimili ya mahindi na alizeti ikiwa na urefu wa sentimita 40 (zulia kunyunyiza mmea wenyewe).

## Wadudu hatari

Ndege na viwavi aina ya 'African Bollworm' ndiyo waharibifu hatari wa alizeti. Viwavi hao hula majani ya kijani kibichi pamoja na mbegu na wanaweza kuhuaribu zao lote shambani.

## Hatua kudhibiti

Uharibifu kutoka kwa ndege waweza kupunguzwa kupitia kuwashtua. Viwavi waweza kudhibitiwa kwa kunyunyizia madawa ya kuuu wadudu yanayopendekezwa.

## Magonjwa makuu

Magonjwa aina mbili kuu ni 'yellow blotch' na 'Sclerotinia'. Ugonjwa wa kwanza husababisha rangi kuwa ya manjano na muundo wa matawi na maua kuharibiwa. Wa pili hupelekea kuoza kwa mimea (mihimili, matawi na hata kichwa cha mmea).

## Kudhibiti

Ule wa kusababisha rangi ya manjano hudhibitiwa kwa kuing'oa na kuchoma mimea iliovamiwa, aidha kunyunyizia dawa (diazinon) ili kuwadhibiti wadudu wanaousambaza. Kubadilisha mimea shambani baada ya kila miaka 5 hukinga aina hiyo ya pili (sclerotinia).